

# FOMU YA KIBALI – YA KUTAMBUA JINA NA MAELEZO YA BINAFSI KWA WATU WENGINE

(Tafadhali chapisha au charaza isipokuwa mstari wa sahihi)

Jina Lako: \_\_\_\_\_

Jina la Shule au Asasi Nyingine Ambayo Umewasilisha Malalamishi Haya Dhidi Yake: \_\_\_\_\_

- Fomu hii inauliza iwapo Ofisi ya Haki za Raia (OCR) inaweza kushiriki jina na maelezo yako mengine ya binafsi OCR inapoamua kuwa kufanya hivyo kutasaidia katika kuchunguza na kusuluhisha malalamishi yako.
- Kwa mfano, ili kuamua iwapo shule ilibagua mtu, mara nyingi OCR huhitaji kutambua jina la mtu huyo na maelezo ya binafsi kwa waajiriwa kwenye shule hiyo ili kuthibitisha ukweli au kupata maelezo ya ziada. OCR inapofanya hivyo, OCR inafahamisha waajiriwa kuwa aina zote za visasi dhidi ya mtu huyo na watu wengine wanaohusiana na mtu huyo ni marufuku. OCR inaweza pia kutambua jina la mtu au maelezo ya binafsi wakati wa mahojiano na mashahidi na ushauri kutoka kwa wataalam.
- Iwapo OCR hairuhusiwi kutambua jina lako au maelezo ya binafsi kama ilivyoelizwa hapo juu, OCR inaweza kuamua kufunga malalamishi yako iwapo OCR itaamua ni muhimu kufichua jina lako na au maelezo ya binafsi ili kusuluhisha ubaguzi dhidi yako.

**DOKEZO:** Ukiwasilisha malalamishi kwa OCR, OCR inaweza kutoa maelezo fulani kuhusu malalamishi yako kwenye vyombo nya habari au umma kwa jumla, likiwemo jina la shule au asasi; tarehe ambayo malalamishi yako yaliwasilishwa; aina ya ubaguzi uliojumuishwa katika malalamishi yako; tarehe ambayo malalamishi yako yalisuluhishwa, kuondolewa au kufungwa; sababu msingi kwa uamuza wa OCR; au maelezo mengine husika. Maelezo yoyote ambayo OCR inatoa kwenye vyombo nya habari au umma kwa jumla hayatajumuisha jina lako au jina la mtu ambaye uliwasilisha malalamishi kwa niaba yake.

**DOKEZO:** OCR inakuhitaji kujibu maombi yake kwa maelezo. Kushindwa kushirikiana na shughuli za uchunguzi na masuluhisho za OCR kunawenza kuchangia kufungwa kwa malalamishi yako.

## Tafadhali tia sahihi sehemu ya A au sehemu ya B (lakini si zote mbili) na urejeshe kwa OCR:

- Iwapo uliwasilisha malalamishi kwa niaba yako mwenyewe, unapaswa kutia sahihi fomu hii.
  - Iwapo uliwasilisha malalamishi kwa niaba ya mtu mwengine, mtu huyo anapaswa kutia sahihi fomu hii.
- KIGHAIRI:** Iwapo malalamishi yaliwasilishwa kwa niaba ya mtu maalum ambaye ni wa chini ya miaka 18 au mtu mzima asiyne na uwezo kisheria, lazima fomu hii itiwe sahihi na mzazi au mlezi wa kisheria wa mtu huyo.
- Iwapo uliwasilisha malalamishi kwa niaba ya kundi la watu, badala ya mtu yeyote maalum, unapaswa kutia sahihi fomu hii.
- A. **Ninaipa OCR kibali changu kutambua utambulisho wangu (na ule wa mtoto wangu mchanga/wadi ambaye malalamishi yamewasilishwa kwa niaba yake) kwa wengine kwa shughuli zaidi za uchunguzi na utekelezaji za OCR.**

---

Sahihi

---

Tarehe

AU

- B. **Siipi OCR kibali changu kutambua utambulisho wangu (na wa mtoto wangu mchanga/wadi ambaye malalamishi yamewasilishwa kwa niaba yake) kwa wengine.** Ninaelewa kuwa OCR inaweza kufunga malalamishi yangu.

---

Sahihi

---

Tarehe

Ninatangaza chini ya adhabu ya kusema uwongo kuwa ni kweli na sahihi kwamba mimi ndimi niliyetajwa hapo juu; na, iwapo malalamishi yamewasilishwa kwa niaba ya mtoto mchanga/wadi, mimi ndimi mzazi/mlezi wa kisheria wa mtu huyo. Tamko hili linatumika tu kwenye utambulisho wa watu na halitumiki kwenye yoyote ya madai yaliyowasilishwa katika malalamishi.